

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3  
Fax Na: 2152820  
(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe  
Kwa Kamishna Jenerali)



08 Barabara ya Kivukoni,  
S. L. P. 80327,  
**11486 DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA UMMA**

KILOGRAM 23.84 ZA DAWA YA KULEVYA AINA YA MIRUNGI ZAKAMATWA TEMEKE

**Dar es salaam, Februari 1, 2023**

Tarehe 26 Januari, 2023 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilifanya operesheni katika wilaya ya Temeke mkoa wa Dar es Salaam na kufanikiwa kukamata kilo 23.84 za dawa ya kulevya aina ya mirungi zikiwa zimehifadhiwa ndani ya nyumba ya **Rhoda Mohamed Salum (48)** ambaye ni mkazi wa Lukongo eneo la Wiles wilayani Temeke akiwa anajiandaa kuzisafirisha kwenda nje ya nchi.

Aidha, tarehe 27 January, 2023 katika dampo la Kituo cha Polisi Chang'ombe, kiasi hicho cha dawa za kulevya kiliteketezwa chini ya uangalizi wa baadhi ya wadau kutoka taasisi zinazotambulika kisheria kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni ya 14 ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. washiriki hao ni pamoja na mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na Dawa za kulevya, Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Temeke, mwakilishi wa Inspekta Jenerali wa Polisi, mwakilishi wa Mkemia Mkuu wa Serikali, mwakilishi kutoka ofisi ya Taifa ya Mashtaka Nchini.

Uteketezaji huo ulifanyika kuendana na matakwa ya kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambacho kinaruhusu uteketezwaji wa baadhi ya dawa za kulevya kwa kuzingatia hali ya hatari ya dawa hizo, kuharibika kwake, athari za kimazingira, ufinyu wa mahali maalum pa kuhifadhi au kwa kuzingatia masuala mengine yanayofanana a hayo. Kwa kuwa mirungi hiyo ilikuwa mibichi, kulikuwepo na uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza uhalisia wake hivyo ilikuwa ni muhimu kuteketezwa kwa dawa hizo.

Upelelezi wa shauri hili bado unaendelea na utakapokamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

Imetolewa na,

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Florence Khambi'.

Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya**